KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 14, Issue 3

18th Shawwâl 1432

16th Sept, 2011

KATIKA MAMBO YENYE KUMFAA MAITI

Na: Abu Ameenah Bilaal Philips

Qur'an imethibitisha misingi miwili ya ujumla yenye kuhusiana na malipo na adhabu ya matendo:

1. Kila mwana-adamu kwa msingi atanufaishwa au kudhuriwa na matendo ambayo yeye ameyatenda. Allah amesema: "**Na kwamba mtu hatapata ila yale aliyoyafanya** [an-Najm 53:39]
2. Hakuna mtu atakayeweza kubeba madhambi ya mwengine. Allah amesema: **"kwamba haichukui nafsi dhambi za nafsi nyengine."** [an-Najm 53:38]

Hivyo basi mtu atakapokufa, fursa yake ya kutenda mema itakuwa imekwisha kwa kufa kwake. Lakini fursa ya kuvuna mazuri kutokana na matendo yaliofanywa kabla ya kufa kwake hubakia.

DU'AA – Maombi ya Waislamu wengine kwa niaba ya aliyekufa yatamnufaisha maiti, kwa ruhusa ya Allah**.** Ikiwa hawakufanya mema hakuna ambaye angeshughulika kuwaombea. Ikiwa walikuwa waovu, maobi ya wengine hayatowanufaisha wao.

Allah awasifu waumini wenye kuwaombea wenzao waliotangulia kabla yao: **"Na (kadhalika wapewe mali hayo Waislamu) waliokuja baada yao (wakawa wanapendana na Waislamu waliotangulia, wanawaombea dua) wanasema: 'Mola wetu tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia (kufa) katika Uislamu. Wala usijaalie katika nyonyo zetu undani kuwafanyia**

THE QUR'AN & SUNNAH HAJJ / 'UMRAH AGENCY

1432HIJRI/ 2011 C.E

Assalaamu 'Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah mwaka huu 1432 Hijri/ 2011, tumeanza Barnaamij ya kupeleka watu Hajj.

Mipangilio Ya Safari

- Kuondoka ni katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Dhul Qa'dah
- Kurudi ni mwisho wa mwezi wa Dhul-Hijjah
- Safari itaanza Mombasa – Nairobi – Jeddah
- Kurudi ni Jeddah – Nairobi – Mombasa
- Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli, Usafiri na Chakula – mara 3 kwa siku tukiwa Mina kwa siku tano)
- Class "B" ni $3800 U.S Dollars / Class "C" ni $3200 U.S Dollars
- Amma mas'ala ya Chakula (Makka na Madinah) kila mtu ni juu yake
- Tutakuwa na Darsa juu ya mas'ala ya Hajj kabla ya kuondoka na tutakapokuwa Makkah
- Tutaandamana na Daktari wetu kutoka hapa Mombasa Insha Allaah

Kwa Maelezo Zaidi

Fika katika Maktaba ya QSS iliyoko ubavuni mwa Tajj Hotel (Duka la tatu baada ya Duka la vitabu vya Dini), au

Wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net, au

Tupigie simu nambari mojawapo ya hizi zifuatazo:

+254 723471820 au +254 721473181, au +254 700365253

YALIYOMO

YENYE KUMFAA MAITI 1 - 2

WENYE KUKADHIBISHA 2 - 3

Waislamu (wenzetu). Mola wetu! Hakika Wewe ni Mpole sana. Mwenye rehema mno'". [al-Hashr 59:10]

Zaidi ya hayo, swala ya jeneza yenyewe inayo ndani yake haswa maombi kwa maiti. Safwan [msimulizi alitaja yakwamba Safwan ibn Abdillah ibn Safwan alikuwa amemuoa ad-Dardaa] alisema: "Nilimzuru Abud-Dardaa (رضي الله عنه) nyumbani kwake Syria, lakini sikumuona yeye humo. Ummud-Dardaa' (رضي الله عنها) akaniuliza [mimi], 'utakwenda kufanya Hajj mwaka huu? Nikasema 'Naam' akasema: 'Tuombee Allah Atuja'alie kheri, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Maombi ya Muislamu kwa nduguye akiwa mbali nae, hujibiwa. Maadamu atakuwa ni mwenye kumuombea nduguye mema, kuna Malaika aliyepewa jukumu la kuwa karibu ya kichwa chake anayesema: 'Ameen, na pia wewe upate kama hayo'. Nikaondoka kuelekea sokoni ambapo nilipokutana na Abud-Dardaa' na yeye akanihadithia hayo hayo kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم)." [Swaheeh Muslim vol.4 p.1429, no.6590]

SAUMU– Saumu alizozikosa maiti zinaweza kufungwa kwa niaba ya jamii zao za karibu. Na saumu zenyewe zaweza kuwa ni za Ramadhaan au za nadhiri.

Aa'ishah (رضي الله عنها) alimnukuu Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: "Yeyote atakayekufa akiwa anadaiwa saumu, msimamizi wake na afunge kwa niaba yake." [Swaheeh Al-Bukhaari, vol. 3, Uk.99 #173 na swaheeh Muslim, vol. 2, Uk. 556, # 2553].

Ibn Abbaas (رضي الله عنه) alisema: "Mtu alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akauliza: 'Ewe Mjumbe wa Allaah,

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

mamangu alikufa akiwa adaiwa mwezi mmoja wa saumu. Nifunge mimi kwa niaba yake? Akamjibu (صلى الله عليه وسلم): "Naam, madeni yenye kudaiwa na Allaah yana haki zaidi ya kulipwa." [Swaheeh Al-Bukhaari, vol.3, Uk.99, no. 174, na Swaheeh Muslim, vol.2, Uk.556, #2554] Katika riwaya nyengine, mwanamke aliuliza kuhusu deni la mama yake la saumu na akapawa jibu kama hilo. [Swaheeh Muslim, vol, 2, Uk.556-7, nos. 2554, 2557-61]

KULIPA MADENI YA FEDHA - Mtu yoyote anaweza kumlipia aliyekufa madeni yake, emma wawe na uhusiano wa kijamii nae au laa. Mbali na hayo, malipo ya madeni ya maiti yaweza kumnufaisha yeye katika kupunguziwa baadhi ya adhabu kwa sababu ya kudharau kulipa madeni hayo.

Jaabir (رضي الله عنه) alisema: "Mtu mmoja alikufa na tukamuosha, tukamtia manukato, na kumvisha sanda. Kisha tukamleta kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ili atuongoze katika kumswalia swala ya jeneza. Tukamuuliza: 'Waweza kumswalia?' Akachukuwa hatuwa mbele kisha akauliza, 'Anayo madeni anayo daiwa?' Tukamjibu: 'Deenar mbili.' Akasema: "Mswalieni swahib wenu' na [nyongeza yaweza kupatikana katika mapokezi mengine ya hadeeth] akaanza kuondoka' Aboo Qataadah (رضي الله عنه) akachukuwa jukumu la kulipa deni hilo, akasema: "deenari mbili ni jukumu langu' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akauliza, "Mwenye kudai ataangaliwa (kulipwa) na maiti ataondokewa na deni?' Akajibu: 'Naam' kwa hivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaswalisha swala ya jeneza. Siku moja baadaye akamuuliza [Aboo Qataadah]: 'Mulifanyaje kuhusu deenar mbili?' Akajibu: 'Si amekufa jana tu!' Siku iliyofuata akarudi kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: 'nimeshalipa,' Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: 'sasa ngozi yake imepoa moto" [Musnad Ahmad vol.3, Uk.330' imeswahihishwa katika Ahkaamul-Janaa'iz Uk.16]

SWADAKA YA WATOTO – Wazazi watanufaika kutokana na matendo yoyote mema yenye kufanywa na watoto wao, bila ya kuwapunguzia ujira wao (watoto). Mtoto mwema huzingatiwa kuwa katika sehemu ya mapato ya wazazi.

'Khalati yake 'Umaarah ibn 'Umayr (رضي الله عنها) alimuuliza Aa'ishah (رضي الله عنها): "Mimi nina yatima aliye chini ya uangalizi wangu. Naweza kula baadhi ya mali yake? Akajibu (Aa'isha) kuwa alimsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: "Miongoni mwa mambo yaliyo mazuri mno ambayo mtu anayoyatumia ni yale yaliyotokana na mapato yake, na mwanawe ni katika mapato yake." [Sunan Abu Daawood vol. 2, Uk.1002,= no.3521. ikaswahihishwa katika swaheeh Sunan Abu Dawood vol. 2, Uk. 674, no. 3013]

Aaishah (رضي الله عنها) alihadithia kuwa mtu alimuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Mamangu amekufa ghafla, na nafikiri kuwa ikiwa angeliweza kuzungumza (kabla ya kufa) angelitoa kitu kwa njia ya swadaka. Nikitoa mimi swadaka kwa niaba yake, atapata ajri?" Akajibu, 'Naam" [Swaheeh Al-Bukhari vol. 2 Uk.266, no.470, swaheeh Muslim, vol. 3 Uk.866, no.4002, na Sunan Abu Daawud, vol. 2. Uk.812, no. 2875]

Aboo Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mtu akifa, matendo yake hukatika (ya mwisho), isipokuwa katika hali tatu: swadaka inayoendelea, ilmu ambayo watu waendelea kunufaika nayo, na mtoto mwema mwenye kumuombea." [Sawaheeh Muslim: vol.3, Uk. 867, no.4005, na Sunan Abu Daawud, vol.2, Uk.812, no.2874].

NENO LA BUSARA

Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema:

"Ni nani miongoni mwenu aliyefunga leo?" Abu Bakr (رضي الله عنه) akajibu: "Mimi nimefunga leo." Akasema: "Ni nani miongoni mwenu aliyehudhuria mazishi leo?" Abu Bakr akajibu: "Mimi nimehudhuria mazishi leo." Akasema: "Ni nani miongoni mwenu aliyemlisha masikini leo?" Abu Bakr akajibu: "Mimi nimemlisha masikini leo." Akasema: "Ni nani aliyemtembelea mgonjwa leo?" Abu Bakr akajibu: "Mimi nimemtembelea mgonjwa leo." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "Sifa hizi hazikusanyiki juu ya mtu mmoja, isipokuwa ataingia Peponi."

[Imepokewa na Muslim, No. 1028]

HUKMU JUU YA MWENYE KUIKADHIBISHA SIKU YA MWISHO, NA NJIA YA KUMSHAWISHI

Na: Shaykh Muhammad ibn 'Uthaymeen (رحمه الله).

SUALI: Ni nini hukmu ya mwenye kukanusha maisha ya siku ya Kiyama? Twawezaje sisi kuwashawishi wenye kuikanusha?

JAWABU: *Alhamdulillaah* — Mwenye kukanusha maisha ya siku ya kiyama ni Kafiri, kwa sababu Allaah amesema:

"Na walisema: 'Hakuna mengine ila maisha yetu (haya tu) ya dunia, wala sisi hatutafufuliwa. Na ungeona (Siku ya Kiyama) watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, akawaambia: 'Je, si kweli haya?' Na wao wakasema: 'Kwa nini? (Ni haki Wallaahi), tunaapa kwa Jina la Mola wetu.' Aseme (Allaah): 'Basi ionjeni adhabu kwa sababu ya kule kukanusha kwenu.'" [al-An'aam 6:29-30]

"Adhabu kali siku hiyo itawathubutukia wanaokadhibisha. Ambao wanaikadhibisha Siku ya Malipo. Wala haikadhibishi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi (anajitia pambani kusudi za kujidai kuikadhibisha). Anaposomewa Aya zetu husema: 'Ni visa vya watu wa kale'. Sivyo hivyo! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao (maovu) waliyokuwa wakiyachuma. Sivyo hivyo! Hakika watazuiliwa siku hiyo na (ne'ma za) Mola wao. Kisha wataingia katika Moto (uwakao). Kisha waambiwe: 'Haya ndiyo mliyokuwa mkiyakadhibisha.'" [al-Mutaffifeen 83:10-17]

"Bali wanakadhibisha Kiyama; na tumewaandalia wanaokikadhibisha Kiyama Moto mkali kabisa. [al-Furqaan 25:11]

"Na wale waliozikufuru Aya za Allaah na kukutana naye, hao ndio watakata tama ya kupata rehema yangu, na hao ndio watakaopata adhabu iumizayo." [al-'Ankaboot 29:23]

Ama kuhusu kuwashawishi

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

wakanushaji hawa, inawezekana kwa njia ifuatayo:

KWANZA:
Kuna riwaya nyingi sana zinazohusiana na mas'ala ya kufufuliwa kutoka kwa Mitume na manabii kwenye vitabu na dini zenye asili ya kutoka kwa Allaah, ambazo zilizokubaliwa na Mataifa yaliyokuwepo. Sasa utakataa vipi haliyakuwa unaamini unayoambiwa yanyotoka kwa watu wa falsafa au mtungaji wa kanuni au mvumbuzi wa fikra, hata kama anayokwambia wewe hayafiki daraja ya uhakika yenye kufikia maandiko yanayozungumzia kuhusu kufufuliwa?

PILI:
Akili inakubali kuhusu uwezekano wa kufufuliwa , kwa sababu chungu nzima:

1. Hakuna awezae kukanusha yakwamba yeye aliumbwa baada yakuwa si chochote. Aliyemuumba na kumfanya awe ni mtu baada yakwamba alikuwa si chochote, ana Uwezo wa kumrudisha tena kwa mara nyengine, kama Alivyosema Allaah:

"Na Yeye ndiye Aliyeanzisha viumbe na ndiye Atakaevirudisha (mara nyingine), na (jambo) hili ni rahisi zaidi Kwake; naye ndie mwenye sifa nzuri mbinguni na katika ardhi, naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima." [al-Room 30:27]

"Siku tutakapozikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za maandishi. Kama tulivyoanza umbo la awali tutalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu yetu. Bila ya shaka sisi ni wenye kufanya (tuyasemayo)." [al-Anbiya' 21:104]

2. Hapana awezae kukanusha utukufu wa viumbe vya mbinguni na ardhini, kwa ajili ya ukubwa wake na uzuri wa ki-maumbile. Aliyeviumba hivyo Ana Uwezo wa kumuumba mwana-adamu. Na ama kuwaumba kwa mara ya pili ni rahisi zaidi Kwake. Amesema Allaah:

"Kwa yakini umbo la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbo la mwana-adamu. (Basi Allaah aliyeumba mbingu na ardhi ndiyo kutamshinda kuwafufua akawapa umbo jengine na uhai mwengine mwana-adamu?) Lakini watu wengi hawajui (ila wanajisemea tu). [Ghaafir 40:57]

"Je! Hawaoni yakwamba Allaah – aliyeziumba mbingu na ardhi na hakuchoka kwa kuziumba - Ana uweza wa kuwafufua wafu? Na'am , hakika yeye ni Muweza wa kila kitu." [al-Ahqaaf 46:33]

"Je, Yule aliyeziumba mbingu na ardhi (mnaona) hana uweza wa kuumba (mara ya pili) mfano wao (wanaadamu)? Kwa nini? Naye ni Mwumbaji Mkuu. Mjuzi (wa kila jambo). Hakika amri Yake anapotaka chochote (kile kitokee) ni kukiambia: 'Kuwa', basi mara huwa." [Ya-Seen 36:81-82]

3. Mtu yoyote mwenye busara aweza kujionea mwenyewe jinsi ardhi inavyo kauka na kufa, ikawa haina mazao yoyote, mara inyeshapo mvua katika ardhi hiyo, inanawiri na mazao yake yakatokeza na uhai ukadhihirika baada ya kwamba ilikuwa imekufa. Mwenye Uweza wa kuihuisha ardhi baada ya kufa ana uwezo wa kuwahuisha na kuwafufua waliokufa. Amesema Allaah:

"Na katika Ishara Zake (kuwa yuko Allaah) ni kwamba unaiona ardhi imedhalilika (kwa kukosa mvua), lakini Tunapoiteremshia maji mara unaiona inataharaki na kumea bila shaka Aliyeihuisha ndiye Mwenye uweza juu ya kila kitu." [Fussilat 41:39].

TATU:
Ukweli wa mambo unashuhudia juu ya fikra yakwamba kufufuliwa ni jambo lisilo na shaka. Matukio yamewahi kushuhudiwa ambamo waliokufa wamefufuliwa. Katika Surat al-Baqarah, Allaah ametutajia kuhusu matukio matano, mojawapo likiwemo:

"(Lakini wale) waliodhulumu (nafsi zao) walibadili kauli isiyokuwa waliyoambiwa. (Badala ya kuomba wasamehewe makosa yao na hawatafanya tena, ndipo walipozidi ubaya). (Kwa hivyo) Tukaiteremsha juu ya wale waliodhulumu adhabu kubwa kutoka mbinguni kwa sababu ya kuasi kwao." [al-Baqarah 2:259].

NNE:
Hikma iliyoko, inaelekeza yakwamba hapana budi kuwepo kufufuliwa baada ya kufa ili kila nafsi ipate kulipwa kulingana na iliyoyatuma. Lau kama si kwa ajili hiyo, kuumbwa kwa wana-adamu hakungekuwa na maana yoyote., hakungekuwa na thamani wala hikma ndani yake, na hakungelikuwa na tafauti yoyote baina ya wana-adamu na wanyama katika maisha ya hapa duniani. Allaah amesema:

"Je, mlidhani yakwamba Tumekuumbeni bure na yakwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa. Ametukuka Allaah, Mfalme wa haki, hakuna aabudiwae kwa haki ila Yeye, Mola wa 'Arshi yenye hishima (kubwa kabisa)." [al-Mu'minoon 23:115, 116]

"Bila shaka Kiyama kitakuja. Nataka kusudi kukificha (Nisiseme lini kitakuja) ili kila nafsi ilipwe kwa yale iliyoyafanya." [Ta-Ha 20:15]

"Nao (wakaapa) kwa jina la Allaah kwa kiapo chao cha nguvu (kwamba) Allaah hatawafufua wafao. Kwa nini (Asiwafufue)? Ni ahadi iliyolazimika Kwake (kwafufua na kuwalipa), lakini watu wengi hawajui. (Atawafufua) ili kuwabainishia yale waliyokhitilafiana, na ili wajue waliokufuru yakwamba wao walikuwa ni waongo. Kauli Yetu kwa kitu Tunachokitaka (kiwe), ni kukiambia: 'Kuwa'; basi kinakuwa tu." [al-Nahl 16:38-40]

"Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: 'Kwa nini? Kwa haki ya Mola wangu nyinyi lazima mtafufuliwa; kisha lazima mtajulishwa mliyoyatenda (na mlipwe kwayo). Na hayo ni sahali kwa Allaah." [al-Taghaabun 64:7]

"Ila wale (watunga mashairi) walioamini, na kufanya vitendo vizuri, na kumtaja Allaah kwa wingi, na wakalipiza kisasi baada ya kudhulumiwa. (Hawa hawahisabiki kuwa wabaya). Na karibuni (hivi) wafanyao dhuluma watajua ni mgeuko (mpinduko) wa namna gani watakaogeuka (watakaopinduka)." [al-Shu'ara 26:227].

ALAMA ZA MWISHO MWEMA NA MBAYA

Na: Shaykh al-Albaani (رحمه الله).

Allaah (سبحانه وتعالى) hupanga alama za dhahiri zenye kuhusiana na kifo cha mtu, katika kuonyesha au kuashiria daraja yake baada ya kufa.

Baadhi ya alama hizi ni ishara za wazi za mwisho mwema. Kufa na (alama) yoyote miongoni mwazo huthibitisha bishara njema kwa aliyekufa - twamuomba Allaah (سبحانه وتعالى) atupe nasi hayo kutokana na Ukarimu wake na Rehma zake zisizo kifani.

Vilevile kuna alama za wazi za mwisho mbaya. Kufa na (alama) yoyote miongoni mwazo huthibitisha ishara mbaya kwa aliyekufa - twamuomba Allaah (سبحانه وتعالى) atulinde na shari hizo.

USHAHIDI WA ISHARA NZURI

KUITAMKA SHAHADA: Mu'aadh (رضي الله عنه) ametuhadithia yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Yoyote ambaye maneno yake ya mwisho ni'**Laa ilaaha illa 'Llaah' ataingia Peponi.**"*

Vilevile Mu'aadh (رضي الله عنه) ametuhadithia yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hapana nafsi yoyote inayokufa haliyakuwa inashuhudia yakwamba hapana mola (wa haki) isipokuwa Allaah na kwamba mimi ni Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم), ikitoka hiyo kwenye moyo wa mu'min, isipokuwa Allaah Huisamehe."*

Amepokea Jaabir yakwamba baada ya kufa Mtume (صلى الله عليه وسلم), 'Umar (رضي الله عنه) aligundua alama za huzuni kwa Talhah Bin 'Ubaydullaah. Akamuuliza, "Una nini, Ewe Abu Muhammad? Mbona waonekana matimutimu na umejaa vumbi tangu alipokufa Mtume (صلى الله عليه وسلم)! Au ni kwa sababu ya kuchaguliwa kwa binamu yako (Abu Bakr kama Khalifah)?" Akajibu, "Laa! Allaah na Atuepushe na hayo!" Na akampongeza Abu Bakr (رضي الله عنه). Kisha akaeleza, "Yote haya ni kwa sababu yakwamba niliisikiya hadeeth kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم); na hapana kilichonizuiya mimi nisimuulize kuhusiana nayo isipokuwa ni kusitasita tu - mpaka akafa! Hii ndiyo sababu ya kuhuzunika kwangu.

Nilimsikiya akisema: *"Kwa hakika, mimi nayajua matamshi fulani ambayo hakuna mtu atakaeyasema katika wakati wa kufa kwake isipokuwa rangi yake ya ngozi hung'ara kwa matamshi hayo, Allaah humuondolea dhiki zake, huiletea roho yake usalama pindi inapotoka kwenye mwili wake, na itakuwa ni muangaza katika daftari lake siku ya kufufuliwa."*

'Umar (رضي الله عنه) akasema, "Mimi nishalijua hilo!" Talhah akamuuliza, "*Alhamdulillaah*! Ni jambo gani hilo?" Akamjibu, "Wewe wayajua matamshi yaliyo makubwa kuliko hayo ambayo kwayo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimshawishi mjombake ayatamke katika mauti yake, *'**Laa ilaaha illa 'Llaah'?"** Akasema Talhah, "Umesema ya kweli! Wallaahi hayo ndiyo mambo yenyewe!"*

KUTOKWA NA JASHO KWENYE BAPA LA USO: Buraydah Bin al-Khaseeb (رضي الله عنه) alikuwa Khurasaan alipomtembelea mtu mgonjwa. Alimkuta kwenye ukingo wa mauti yake, na akaona yakwamba bapa lake la uso lilikuwa limejaa majasho. Basi akasema, *"Allaahu Akbar!* Mimi nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: *"Mu'min hufa na bapa la uso lenye jasho."*

KUFA KATIKA SIKU YA IJUMAA

'Abdullaah Bin 'Amr (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hapana Muislamu yoyote atakaekufa katika siku ya Ijumaa au usiku wa Ijumaa, isipokuwa hulindwa kutokana na fitna za Kaburi."*

KUFA SHAHIDI KATIKA UWANJA WA VITA

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Wala usiwadhani wale waliouwawa katika njia ya Allaah kuwa ni wafu (maiti). Bali wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao. Wanafurahia aliyowapa Allaah kwa fadhila Zake; na wanawashangilia wale ambao hawajajiunga nao, walio nyuma yao, (wako ulimwenguni, bado hawajafa); yakwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Wanashangilia ne'ema na fadhila za Allaah, na kwamba Allaah hapotezi ujira wa wanaoamini."** ['Aali-'Imraan 3: 169-171].

Al-Miqdaam Bin Ma'd Yakrib, 'Ubaadah Bin as-Saamit, na Qays al-Juthaami (رضي الله عنهم), wote wamepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Shahidi mbele ya Allaah hupewa fadhla sampuli saba: Husamehewa kwa bubujiko la kwanza la damu, huonyeshwa mahala pake peponi, hulindwa na adhabu ya kaburi, huokolewa kutokamana na Kufazaika Kukubwa (Siku ya Malipo), hupambwa na mapambo ya Imaan, huozwa wanawake wa al-Hur ul-'In (wanawake wazuri wa Jannah), na huruhusiwa kuwaombea watu sabiini miongoni mwa jamaa zake."*

Mmojawapo wa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amepokea yakwamba mtu mmoja aliuliza, "Ewe Mjumbe wa Allaah, ni kwa nini yakwamba waumini wote hupewa mitihani kwenye makaburi yao, isipokuwa mashahidi?" Akajibu (صلى الله عليه وسلم): *"Mwangaza unaomulikwa na mapanga juu ya kichwa chake ni mtihani unaomtosha."*

Inatakiwa kufahamika hapa yakwamba Muislamu yoyote mwenye kutamani kwa ikhlasi kufa akiwa ni shaheed atapewa hilo, hata kama hatokufa kwenye uwanja wa vita. Abu Hurairah na 'Umar (رضي الله عنهم) wamepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Yoyote mwenye kumuomba Allaah kwa Ikhlaas kufa Shaheed, Allaah atampa daraja za Mashaheed, hata kama atakufa kwenye kitanda chake."*

Kwa mukhtasar, ifuatayo ni orodha ya ishara nzuri za kufia:

- ◊ Kufa kwa ugonjwa wa Tauni.
- ◊ Kufa kwa maradhi ya tumbo.
- ◊ Kufa kwa kuzama baharini.
- ◊ Kufa kwenye maporomoko ya nyumba.
- ◊ Kifo cha mwanamke kutokana na mazazi.
- ◊ Kifo kutokana na kuteketea na moto.
- ◊ Kifo kutokana na Pleurisy.
- ◊ Kifo kutokana na T.B
- ◊ Kufa kwa kutetea haki yako.
- ◊ Kufa kwa ajili ya kutetea familia yako.
- ◊ Kufa kwa ajili ya kutetea Dini.
- ◊ Kufa wakati wa kujihami.
- ◊ Kufa ukiwa umesimama kama mlinzi kwenye njia ya Allaah (Jihaad).
- ◊ Kufa wakati unapofanya wema.
- ◊ Kuuwawa na kiongozi dhalimu.
- ◊ Kuuwawa.
- ◊ Kusifiwa kwa mazuri na Waislamu walio wema.

Kwa mukhtasar, ifuatayo ni orodha ya ishara mbaya za kufia:

- ◊ Kufa haliyakuwa katika ukafiri.
- ◊ Kufa haliyakuwa unafanya kitendo cha ma'asiya.
- ◊ Kukataa kuitamka shahada wakati wa kufa.
- ◊ Kulaumiwa aliyekufa na Waislamu walio wema.
- ◊ Mlevi mzoefu.
- ◊ Kuwatendea wazazi ubaya.
- ◊ Ukosefu wa kuwa na Ghera na Familia yako.
- ◊ Kifo cha Ghafla.
- ◊ Kufa kabla ya kutubia kutokana na madhambi makubwa.